

NI VYEMA MTEULE AKAWA NA UFAHAMU HUU WAKATI WAKE
WA SAFARI YA KUMNGOJA BWANA YESU.
MAANDIKO: AYUB. 19:25-27.

1. UTANGULIZI

“For I know that my Redeemer and Vindicator lives, and at last he will stand upon the Earth” Leo tunapoelekea katika kumaliza mwaka 2021, nimependa sana wapendwa tuushiriki sote kwa pamoja **ufahamu** wa Kiroho wa hali ya juu aliokuwa nao ndugu yetu Ayubu kuhusu mwokozi wake (Mungu wake).

- Katika nyakati za Biblia Agano la Kale, mtu anayeitwa Mkombozi (Mwokozi) alikuwa lazima awe ni ndugu wa **karibu katika ukoo ambaye** kwa upendo mkubwa alikuwa anasimama ili **kumlinda; kumtetea pamoja na kutoa msaada (kumsaidia)** ndugu yake ambaye anapitia taabu na dhiki nyingi **Law. 25:25, Kumb. 25:5-10 (soma pia Ruth.3:1-13, Ruth.4:1-15.** Hii ndiyo maana halisi katika lugha ya Kiyahudi wakati **Ampl. Bible ilipokuwa inaandika “For I know that my redeemer and vindicator lives, and at last he will stand upon the earth”** yaani Ayubu alimfahamu Mungu kama ndugu yake wa karibu na anayeishi, na kwamba baadaye lazima tu atasimama ili kumwokoa pamoja na kumthibitisha (kumbariki tena). Huu ni ufahamu wa hali ya juu sana aliokuwa nao Ayubu na kisha kuukiri mbele ya maadui zake waliokuwa wakimdhahiki na kumkejeli.

- 2. Kwa sehemu kubwa Ayubu alikuwa amejifunza tabia ya Mungu ya kuwakomboa watu wake wanapokuwa katika taabu kubwa na kuwathibitisha baadaye kama alivyofanya kwa wana wa Israel huko Misri. **Kut. 6:2-9** na Ayubu kama nilivyosema huko nyuma alimwona Mungu kuwa ndiye ndugu yake wa pekee na aliye karibu naye kuliko ndugu mwingine yeyote, na kwa sababu alifahamu uweza wa mkono wake wa kuume katika kutetea na kisha kubariki watu wake, Ayubu

hakutetereka hata alipokuwa anapitia katika dhiki nyingi za maisha na mashambulizi ya adui

Note: Kwa mujibu wa Neno la Mungu, wakati mwingine wateule wanashindwa kabisa kusikiliza kweli ya maneno ya Mungu pamoja na watumishi wake kwa sababu mbili kubwa ambazo ni hizi;

a. **Watu wanakuwa wamejaa uchungu moyoni mwao (yaani wanajiuliza huyu Mungu alikuwa wapi mpaka haya yote yanatupata!! *Kut.6:9, Waam.6:11-13 na Zab.89:49*. Hii ni sababu kuu sana hata kwa wateule wengi katika kizazi chetu**

- Ndiyo sababu Ayubu anakuwa na ufahamu wa tofauti kabisa kiroho kwani wakati mabaya mengi yamempata katika maisha yake ambayo sote tunayafahamu – kwanza hakumlalamikia Mungu!! Wala kuwa na uchungu moyoni mwake; na badala yake anamtukuza Mungu. ***Ayub.1:20-22, 19:25-27!!*** Na zaidi sana kwa kuwa anamfahamu kama ndugu yake wa karibu sana, anafahamu kwamba upo wakati wake tu lazima ambao atasimama na kumkomboa na kumthibitisha.

b. Jambo lingine linalofanya watu wa Mungu waache kumsikiliza Mungu na watumishi wake ni **ile hali ya utumwa mgumu wanaokabiliana nao kila wakati. *Kut.6:9 (Kut.5:1-23,6:1)***

- Ni kazi ngumu sana kumwambia mtu hata leo kwamba Yesu anainua mtu kutoka chini na kumbariki wakati maisha yake tangu alipoamini hajawahi kuona nafuu yoyote ya mafanikio!! Kumwambia mtu kwamba Yesu anaponya magonjwa yote wakati yeye magonjwa yamejaa kwake!! Lakini Ayubu wakati ameshushwa chini kabisa na ibilisi na anateseka sana na majipu mabaya mwili mzima, bado anafahamu fika Mungu kama ndugu yake wa karibu sana atamwokoia katika hali zote hizo na kisha kumthibitisha (kumbariki). **Hakika ufahamu wa Ayubu kiroho ulikuwa wa kiwango cha hali ya juu sana hadi Mungu anakiri hivyo. *Ayub.42:7-9***

3. **Mungu ataendelea kuwa Mungu hata kama atachelewa kufanya kama tunavyotaka sisi leo;** Hata kama tutamwomba mvua na isinyeshe bado ataendelea kuwa Mungu, hata kama tutalala na njaa au kutojenga nyumba nzuri au wapendwa wetu kuugua na wengine hata kufa kabisa au hata kama tutadhulumiwa haki zetu na watawala au kukandamizwa na walio juu yetu au mimba kuharibika au kutoolewa/kuoa au kuvamiwa na majambazi n.k bado Mungu ataendelea kuitwa Mungu. Tunalotakiwa kufahamu kwa kina ni hili alilofahamu Ayubu katika **Ayub.19:25(b) hatimaye Mungu atasimama!!**

- Neno hatimaye (**At last**) linatabiri hali ya mteule ya baadae na siyo hali aliyonayo sasa hivi (leo hii)!!
- Ayubu alipata neema ya kuiona hali yake ya baadaye kutokana na ukaribu wake na Mungu aliyemfahamu kama ndugu yake wa karibu mno jambo lililomfanya asimame imara bila kumkosea hata alipokuwa anapitia katika utumwa mgumu sana wa magonjwa.
- Kama Bwana atatupa ufahamu nasi wa kumfahamu Mungu kama rafiki yetu wa karibu kuliko ndugu yetu wa mwili, yeyote na tukafahamu hali yetu ya baadaye tutakavyokuwa, hakika hatutayumbishwa tena na imani feki nyingi zinazovuma leo wala kukatishwa tamaa na dhiki tunazokabiliana nazo siku kwa siku!! **2Kor.12:7-11, Rum. 8:31-39 na Ufun.19:1-16. Bwana tufunulie ufahamu wetu ili tufahamu kwa kina jinsi ulivyo Mwokozi wetu na mthibitishaji wetu hata kama leo tunaishi kwa imani.**

Na

Askofu Dr. L. Mwizarubi

Dec 2021